

MWONGOZO WA KUHITIMUWA SHULE YA JEFFCO NA MATAYARISHO YA BAADA YA SHULE YA UPILI

(MATAYARISHO YA WANAFUNZI KUJIUNGA NA CHUO KIKUU NA KUINGIA KATIKA AJIRA)

KUKAMILISHA SAA 23 ZA MASOMO



mwanafunzi amepata alama kwenye kozi zinazohitajika za kielimu

KUONYESHA UTAYARI WA KUJIUNGA NA CHUO KIKUU NA KUINGIA KATIKA AJIRA



anaweza kutumia ujuzi wa Kusoma, Kuandika & Kuwasiliana na Hisabati

KUHITIMU KWENYE SHULE YA UPILI



mwanafunzi yuko tayari kufuata malengo ya baada ya shule ya upili

Wanafunzi wa darasa la wahitimu la 2022 na kuendelea sharti wakamilishe angalau saa 23 za masomo katika kozi zinazohitajika na waonyeshe Utayari wa Kujiunga na Chuo Kikuu na Kuingia katika Ajira kwa angalau kipimo kimoja katika Kusoma, Kuandika na Kuwasiliana na kipimo kimoja katika Hisabati.

Kazi 3 kati ya 4



ZINAHITAJI ELIMU AU MAFUNZO ZAIDI YA SHULE YA UPILI

Maisha baada ya shule ya upili yamebadilika:

- Wanafunzi wanahitaji ujuzi muhimu unaofikia viwango vya biashara, tasnia na elimu ya juu.
- Masharti haya hutayarisha wanafunzi wetu kwa malengo ya kitaaluma ya baada ya shule ya upili.
- Wanafunzi, familia na shule zikifanya kazi pamoja, tunaweza kutayarisha wanafunzi kufanikiwa baada ya shule ya upili bila kujali taaluma wanayochagua.



Maonyesho mengi ya matayarisho ya wanafunzi kujiunga na chuo kikuu na kuingia katika ajira yanapatikana mapema kuanzia darasa la 9. Jedwali lililo hapa chini linaangazia chaguo mbalimbali na alama ya(z) kawaida zaidi zinapotolewa. Wasiliana na shule yako kwa maelezo mahususi zaidi.

Darasa	AN	ACT	AWK	AP	ASVAB	CE/DE	DC	IC	IB	SAT
12										
11										
10										
9										
Inapatikana Mara nyingi Inapatikana Wakati Mwingine Haipatikani sana	AN - Accuplacer Next ACT - American College Test AWK - ACT WorkKeys AP - Advanced Placement				ASVAB - Armed Services Vocational Aptitude Battery ASVAB - Armed Services Vocational Aptitude Battery DE - Dual Enrollment			DC - District Capstone IC - Industry Certificate IB - International Baccalaureate SAT - Scholastic Aptitude Test		

Dhamira yetu ni kutoa elimu bora ambayo inawatayarisha watoto wote kwa maisha bora ya baadaye.



ALAMA ZA KOZI ZINAZOHTAJIKA

Wanafunzi wanahitajika kukamilisha saa 23 za masomo yaliyoonyeshwa hapa chini.

SOMO	Alama za Jeffco	Alama za HEAR ^a
Kusoma, Kuandika na Kuwasiliana	4	4
Hisabati	3 ^b	4
Sayansi	3 ^c	3
Somo la Maarifa ya Jamii	3.5 ^d	3
Somo la Michezo ya Kimwili	0.5	Hakuna
Sanaa ya Ubunifu/Vitendo	0.5	Hakuna
Lugha ya Ulimwengu/Kigeni	Haitumiki	1
Masomo ya ziada	8.5	2
JUMLA	23	Haitumiki

a. Mapendekezo ya Kusajiliwa kwenye Elimu ya Juu kwa vyuo vikuu vya umma vya miaka minne vya Colorado; vyuo vikuu vya kibinafsi huweka viwango vyao vya usajili

b. Angalau aljebra 1, jiometri na kozi moja ya ziada katika au juu ya jiometri

c. Alama tatu zinazohusiana na maabara na zinafikia viwango vya mchakato na maudhui zinahitajika

d. Jiografia, historia ya Marekani, historia ya dunia, serikali ya Marekani, uchumi



MAONYESHO YA MATAYARISHO YA WANAFUNZI KUJIUNGA NA CHUO KIKUU NA KUNINGIA KATIKA AJIRA (PWR)

Sharti wanafunzi waonyeshe utayari wa angalau kipimo kimoja katika Kusoma, Kuandika na Kuwasiliana na kipimo kimoja katika Hisabati.

PWR CHAGUO ^a	Kusoma, Kuandika na Kuwasiliana	Hisabati
Accuplacer Next	241/Kusoma au 236/Kuandika	255/AR, au 230/QAS ^b
ACT	18	19
ACT WorkKeys	Bronze	
Advanced Placement ^c	2	2
ASVAB	31	
Concurrent/Dual Enrollment	Alama ya Kufaulu	Alama ya Kufaulu
District Capstone	Kufaulu	Kufaulu
Industry Certificate	Imekamilishwa	
International Baccalaureate ^c	4	4
SAT ^d	470	480 ^e
Performance Based Assessment (katika maendeleo)	Kiwango cha Kitaifa	Kiwango cha Kitaifa

a. Wasiliana na shule yako ili kujua ni chaguo gani kati ya zilizo hapo juu zinazotolewa

b. Hesabu (AR); Uwezo wa Kutumia Dhana na Ujuzi wa Kihisabati katika Maisha Halisi, Aljebra na Takwimu (QAS)

c. Maonyesho mengine yanaweza kuhitajika ikiwa alama za mthani zikiwasilishwa baada ya tarehe ya makataa

d. Wanafunzi wote wanatakiwa kufanya SAT katika mwaka wao wa tatu katika shule ya upili

e. Bodi ya Jimbo la CDE ilibadilisha alama zinazopasawa kufikiwa ili kuonyesha utayari wa Hisabati kwa SAT kutoka 500 hadi 480 kwa madarasa ya 2025 na 2026.

Pata maelezo zaidi [kwenye https://tinyurl.com/JeffcoGrad](https://tinyurl.com/JeffcoGrad)